TANGAZO LA SERIKALI NA. 208 la tarehe 22/3/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 6(1) na 16(1))*

## SHERIA NDOGO YA UTAMADUNI NA ADA YA VIBALI VYA BURUDANI YA HALMASHAURI YA MJI MAFINGA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Utamaduni na Ada ya Vibali vya Burudani ya Halmashauri ya Mji Mafinga ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Mji Mafinga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni kiasi cha fedha kinachotozwa na Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"eneo la burudani" maana yake ni mahali popote ambapo shughuli za burudani zinafanyika;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji Mafinga;

"kibali cha burudani" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya shughuli

za burudani;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mafinga au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"shughuli za burudani" maana yake ni sherehe, shughuli yoyote ya kijamii, sanaa na utamaduni, michezo na muziki.

Utaratibu wa kuomba kibali

4. Mtu anayekusudia kufanya shughuli za burudani katika eneo la Halmashauri anapaswa kuomba kibali kwa Mkurugenzi kwa kujaza fomu maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza na kulipa ada iliyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Vigezo vya utoaji kibali

5.-(1) Halmashauri itatoa kibali iwapo itajiridhisha na masuala yafuatayo:

(a) shughuli ya burudani inayoombewa kibali haitasababisha uvunjifu wa amani;
(b) eneo linaloombewa kibali cha kufanyia shughuli za burudani linaruhusiwa kwa shughuli inayoombewa kibali;
(c) ukumbi wa burudani una usalama wa kutosha ikiwa ni pamoja na kuwepo madirisha ya kutosha ya kuingiza na kutolea hewa, milango ya dharura, umeme na milango inayofunguka kwa urahisi wakati wa dharura; na
(d) shughuli za burudani kuendana na maadili ya kitanzania.

(2) Endapo maombi ya kibali yatakataliwa, Halmashauri itamtaarifu mwombaji kwa maandishi na kutoa sababu za kukataa kutoa kibali hicho.

(3) Baada ya kupata kibali cha kufanya shughuli za burudani, mwombaji atapaswa kuwasilisha nakala ya kibali kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

Wajibu wa

6.-(1) Mmiliki wa ukumbi wa muziki, burudani au

mmiliki wa ukumbi, nk.

baa atakuwa na wajibu wa-

(a) kupiga muziki kwa kiwango cha sauti cha kawaida bila kuathiri watu wanaozunguka eneo la ukumbi huo wa muziki;

(b) kuhakikisha wanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane haingii katika kumbi hizo; na

(c) kuonesha picha mjongeo au sinema kwa sauti ya chini bila kuathiri majirani wanaomzunguka.

(2) Mmiliki wa ukumbi wa muziki, burudani au baa atakayekiuka masharti ya aya hii anatenda kosa.

Mkusanyiko wa watoto

7.-(1) Mtu hatakusanya watoto kwa ajili ya shughuli yoyote ndani ya Halmashauri bila kibali cha maandishi kutoka kwa Halmashauri.

(2) Mkusanyiko wowote wa watoto uliopata kibali cha Halmashauri kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) utakuwa ni siku za mapumziko na utaanza saa nne kamili asubuhi na utamalizika kabla ya saa kumi na mbili jioni.

(3) Mtu aliyepata kibali cha mkusanyiko wa watoto atakuwa na wajibu wa kuhakikisha usalama wao kipindi chote cha mkusanyiko na kuhakikisha wanatawanyika kwa usalama kutoka katika eneo la mkusanyiko.

(4) Mzazi, mlezi au mtu yeyote mwenye mamlaka juu ya mtoto anayeruhusu au kusababisha kwa uzembe mtoto kuhudhuria mkusanyiko usio na kibali cha Halmashauri, anatenda kosa.

Muda wa burudani

8. Muda wa shughuli za burudani utaanzia saa kumi kamili jioni hadi saa sita kamili usiku kwa siku za kazi, na kuanzia saa saba kamili mchana hadi saa sita kamili usiku siku za jumamosi, jumapili na siku za sikukuu.

Vibali visivyotozwa ada

9. Maombi ya kibali kwa shughuli zifuatazo hayahitaji kulipiwa ada:

(a) mikusanyiko ya kidini;

(b) misiba na mazishi; na
(c) michezo ya watoto isiyotozwa.

Muziki unaoleta kero

10. Mtu mwenye leseni ya biashara au kibali cha shughuli za burudani hatapiga muziki unaoleta kero kwa majirani na jamii kwa ujumla katika eneo lake la biashara.

Usafi wa mazingira

11.-(1) Mtu atakayeendesha shughuli za burudani ndani ya mamlaka ya Halmashauri atalazimika kufanya usafi ndani au nje ya eneo lililotumika katika shughuli ya burudani kwa kuondoa uchafu wote uliosababishwa na shughuli hizo.

(2) Mtu anayekiuka masharti ya aya ndogo ya (1) atawajibika kulipa gharama ya uchafuzi wa mazingira kadiri zitakavyokadiriwa na Halmashauri na gharama nyingine ambazo Halmashauri itaingia katika kuondoa uchafu huo.

Mamlaka ya kufanya ukaguzi

12.-(1) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, afisa mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au mahali popote panapofanyika shughuli za burudani kuanzia saa saba kamili mchana hadi saa sita kamili usiku kwa lengo la kukagua iwapo shughuli hiyo ina kibali au inafuata masharti ya kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Katika kutekeleza mamlaka yake chini ya aya ndogo ya (1), afisa mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kutoa maelekezo yoyote ikiwa ni pamoja na kusitisha shughuli za burudani kulingana na hali itakayobainika baada ya ukaguzi kufanyika.

Ukamataji wa vifaa

13.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukamata vifaa vyovyote vitakavyokutwa katika shughuli ya burudani ambayo haina kibali au inayoendeshwa bila kuzingatia masharti ya kibali.

(2) Vifaa vitakavyokamatwa kwa mujibu wa aya

ndogo ya (1) vitachukuliwa na kuhifadhiwa katika ofisi za Halmashauri au eneo lolote litakaloamuliwa na Halmashauri.

(3) Mmiliki wa vifaa vilivyokamatwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii anaweza kuomba kurejeshewa vifaa hivyo ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kukamatwa na baada ya hapo Halmashauri inaweza kuuza vifaa hivyo kwa mnada baada ya kuomba na kupata kibali cha mahakama.

(4) Mtu anayeomba kurejeshewa vifaa vilivyokamatwa chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa gharama za ukamataji, usafirishaji na ulinzi.

Makosa

14.-(1) Mtu anatenda kosa endapo mtu huyo-

(a) anapiga muziki unaoleta kero kwa majirani;
(b) anaonesha picha mnato au picha mjongeo ambazo maudhui yake ni kinyume na maadili;
(c) anamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru wa shughuli za burudani;
(d) anamzuia Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(e) anashindwa, anadharau, anakwepa au anakataa kulipa ada au ushuru wa shughuli za burudani au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii ;
(f) ni mzazi au mlezi wa mwanafunzi au mtoto chini ya umri wa miaka kumi na nane aliyekutwa katika shughuli za burudani wakati wa usiku;
(g) anaruhusu watoto, wanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane kuingia katika shughuli za burudani kinyume na aya ya 7; au
(h) anafanya shughuli ya burudani katika eneo la Halmashauri bila kibali.

Adhabu

15. Mtu anayetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilisha kosa

16. Mkurugenzi anaweza kumtaka mtu aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kulipa kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi katika fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI
SEHEMU YA KWANZA
(Taarifa za Mwombaji)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la mwombaji<br><br>............................................................. | 2. Anwani ya mwombaji<br><br>......................................... |
| 3. Aina ya shughuli<br><br>.............................................................. | 4. Eneo analokusudia kufanya shughuli<br><br>........................................... |

| | |
|---|---|
| 5. Muda wa kuanza<br><br>............................................................. | 6. Muda wa kumaliza<br><br>..................................................... |
| 7. Ada ya kibali (Shilingi)<br><br>.......................................................... | 8. Namba ya stakabadhi ya malipo<br><br>................................................. |
| 9. Saini……………………………… | 10. Tarehe………………….... |

SEHEMU YA PILI
(Kwa Matumizi ya Ofisi tu)

| | |
|---|---|
| 1. Maombi namba<br><br>..................................... | 2. Ada ya kibali shilingi<br><br>....................................................... |
| 3. Namba ya stakabadhi ya malipo<br><br>.................................................. | 4. Tarehe ya malipo<br><br>....................................... |
| 5. Jina la afisa aliyepokea malipo<br><br>................................................... | 6. Saini<br><br>...................................... |
| 7. Muhuri | |

Maoni ya Afisa Mwidhiniwa: - *Nakubali/Sikubali (*futa isiyohusika*)

Sababu: ……………………………..…………………………………………

Jina:………………………………Saini: ……………Tarehe………………..

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

ADA ZA KUENDESHA SHUGHULI ZA BURUDANI, UTAMADUNI NA SANAA

(a) Ada ya Kibali cha Burudani

| Namba | Aina ya Burudani | Ada kwa Kila Onesho/Tukio (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Onesho la muziki | 50,000/= kwa siku |
| 2 | Onesho la michezo ya kuigiza | 30,000/=kwa siku |
| 3 | Muziki wa disko | 30,000/=kwa siku |
| 4 | Muziki/nyimbo za asili | 30,000/=kwa siku |
| 5 | Sherehe za mashirika na taasisi mbalimbali | 30,000/=kwa siku |
| 6 | Onesho la sinema | 30,000/=kwa siku |
| 7 | Sherehe mbalimbali | 20,000/=kwa siku |
| 8 | Kurekodi video | 30,000/=kwa mkanda |
| 9 | Banda la video | 20,000/=kwa mwezi |
| 10 | Tamasha la ngoma za asili | 20,000/=kwa siku |
| 11 | Matumizi ya eneo la wazi | 30,000/=kwa siku |
| 12 | Dance | 50,000/= kwa siku |
| 13 | Maonesho ya sanaa/vichekesho (comedy) | 50,000/= kwa siku |

| | | |
|---|---|---|
| 14 | Pool | 20,000/= kwa mwezi |
| 15 | Ushuru wa tiba asilia | 30,000/= kwa mwaka |
| 16 | Bahati nasibu | 20,000/= kwa mwezi |
| 17 | Korokoro/Tombola/Fete | 20,000/= kwa mwezi |
| 18 | Michezo ya kubahatisha | 30,000/= kwa mwezi |
| 19 | Bahati nasibu ya sanduku | 50,000/= kwa mwaka |
| 20 | Studio ya kurekodi kazi za sanaa | 30,000/= kwa mwezi |
| 21 | Sanaa za ufundi | 10,000/= kwa mwezi |
| 22 | Mashindano ya urembo | 50,000/= kwa tukio |
| 23 | Matangazo mitaani kwa kutumia spika | 30,000/= kwa siku |
| 24 | Matangazo madogo ya biashara | 30,000/=kwa mwezi |
| 25 | Kibali cha kutoa huduma kwa tiba asili | 30,000/=kwa tukio |
| 26 | Usajili wa vikundi vya sanaa | 25% ya malipo ya BASATA |
| 27 | Kuendesha michezo ya magari, pikipiki, baiskeli na wanyama | 50,000 /= kwa siku |

(b) Ushuru kwa watoa huduma kwenye burudani

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Washereheshaji | 10,000/= kwa tukio |
| 2. | Mpiga picha za mnato | 10,000/=kwa tukio |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Mpiga za mjongeo | 10,000/= kwa tukio |
| 4. | Wapambaji wa kumbi za burudani | 20,000/= kwa tukio |
| 5. | Muziki (Dj) | 10,000/= kwa tukio |
| 6. | Mtoa huduma ya chakula | 20,000/=kwa tukio |
| 7. | Wamiliki wa kumbi za starehe | 50,000/= kwa tukio |

______________

JEDWALI LA TATU

______________

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 16)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA MAKOSA

Mimi …………………………………………………… nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji Mafinga, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …… ya Sheria Ndogo ya Utamaduni na Ada Vibali vya Burudani ya Halmashauri ya Mji Mafinga ya Mwaka 2024.

Nipo tayari kulipa kiasi cha ada ninayodaiwa pamoja na faini.

Nathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa mimi mwenyewe kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Leo tarehe …………………..ya mwezi …………… mwaka …………………
Jina: ……………………………………….
Saini: …………………………….

MBELE YA:
Jina: …………………………………
Wadhifa: …………………………….
Saini: ………………………………..
Tarehe: ………………………… …

Lakiri ya Halmashauri ya Mji Mafinga imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji Mafinga uliofanyika Tarehe 14 mwezi 02 Mwaka 2023 na kushuhudiwa Lakari hiyo ikigongwa mbele ya ;-

AYOUBU J. KAMBI
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Mji Mafinga*

REGNANT Z. KIVINGE
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Mji Mafinga*

NAKUBALI

L.S

DODOMA
31 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais*
*Tawala za Mikoa Na Serikali za Mitaa*